



Welcome letter for ESL at Lynchburg City Schools – Swahili

Kwa Mzazi/Msaidizi,

Kwanza kabisa tunakukaribisha katika mji wa Lynchburg. Umepata barua hii kwa sababu mtoto wako ni bahadhi ya wale wameingia katika mashule ya mji wa Lynchburg, natunaelewa yakwamba lugha ya Kingereza siyo lugha yake ya kwanza. Tunamtarajia mtoto wako kufaulu, na tumo tayari kumsaidia kuelewa na Kingereza. Usaidizi wako kwa maendeleo ya mtoto wako ni ya muhimu kwetu, kwa hivyo tunaomba ruhusa kumuandikisha mtoto wako kwa masomo ya Kingereza (ESL). Pamoja na barua hii, ni fomu ya kuandikisha mtoto wako.

Kabla ya kujaza fomu hii, tunaeleza mpango wa masomo ya Kingereza (ESL). Wanafunzi wa masomo ya Kingereza (ESL) watakuwa wameandikishwa kwa muhula wa darasa na wenzio: miaka tano(5) ni nasari (kindergarten), miaka sita ni darasa la kwanza, nakadhalika. Pamoja na masomo haya ya kawaida, wanafunzi wanao chukua masomo ya Kingereza (ESL) watasoma nusu-saa ya kingereza kila siku. Wanafunzi watapangwa kulingana na umri au ujuzi wao. Kabla ya kuandikishwa kwa darasa, walimu na wataalamu watapeana mitihani kutambua ujuzi wa Kingereza wa kila mwanafunzi.

Kuna viwango vinne (4) vilio andaliwa na wakuu wa masomo katika state ya Virginia. Kila kiwango kinaonesha ujuzi wa kuelewa, kusikia, kuongea, kusoma na kuandika Kingereza. Ifuatayo ni maelezo ya viwango:

Kiwango cha Kwanza (1) – Wanafunzi wataanza kuelewa maneno yanao tumiwa kilasiku, kujibu wakitumia vipande vya maneno kwa mistari, kutambua maneno, wakuaona na macho, kuelewa wakisomo na kuandika serufi (ya juu na ya chini).

Kiwango cha pili (2) – Wanafunzi wataanza kuelewa utumizi wa tenzi, kuzugumza kwa ufupi, kuelewa hadithi fupi, kuelewa fununu za mambo mhimu, kuandika hadithi fupi, kuandika ukamilifu na utimilivu wa maneno, na utumiaji wa lugha ingawa makosa kadhaa yatakuwepo.

Kiwango cha tatu (3) – Wanafunzi wataanza kuelewa na upana wa utumiaji wa aina nyingi za maneno kwa lugha, maumbile na utungaji wa maneno, ujuzi wa kujieleza kwa aina nyingi za maisha, kuzungumza kutumia lugha kwa wakati ufaao, kuelewa misemo ya lugha, kuandika ukurusa fupi, kutumia tenzi ifaayo, na kuandika mawazo yakifuatana kwa utaratibu.

Kiwango cha nne (4) – Wanafunzi wanaanza kuelewa utumiaji wa Kingereza shuleni na nyumbani kwa kiwango sawa, kuzungumza na wengine ingawa makosa kadhaa yatakuwepo, kuelewa na viwango kadhalika wakitumia njia mbali mbali za masomo, na kuandika lugha kama wenzio wale wazungumzao Kingereza kama lugha ya mama.

Tunahakiki mtoto wako atafahidi kuwa kwa darasa ya masomo ya Kingereza(ESL). Nia yetu ni kumsaidia mtoto wako kujua kingereza. Mtoto wako atawaza na kuelewana na wanafunzi wenzake na walimu, na kufaulu shuleni.

Unaweza kumsaidia mtoto wako kwa kumuweka moyo. Endelea kutumia lugha yako ya kawaida nyumbani, na kumuhimiza mtoto wako kusoma kwa lugha hii. Kuelewa kusoma na kuandika kwa lugha ya mama kutamsaidia kuelewa, kusoma na kuandika kwa lugha ya pili. Utafiti umeonesha watoto wanaweza faulu kwa lugha mbili pamoja. Lakini, kujifunza lugha ya pili huchukua wakati. Pia utafiti waonesha kwa wastani, inaweza kumchukua mwanafunzi miaka tano mpaka saba kufika kiwango cha kuzungumza Kingereza kama wale waliojifunza kama lugha yao ya kwanza. Tuko hapa kwa usaidizi wako.

Asante,

Viongozi wa Mashule, mji wa Lynchburg ESL



**Ruhusa ya kumpa Mtihani na Kuandikisha
Mwanafunzi alio na Upunguvu wa Kuelewa Kingereza (ESL)
(Fomu hii itadumishwa kwa faili ya mwanafunzi)**

Jina la Mtoto _____

Jina la Mzazi/Msaidizi wa mtoto _____

Lugha mtoto anayo zungumza nyumbani, isio Kingereza (lugha ya mama)?

Tafadhali chagua mojawapo kuruhusu mtoto wako kupewa mtihani wa kuonesha kiwango chake cha kuelewa Kingereza.

- Napeana ruhusa kwa idara ya Elimu ya mji wa Lynchburg kumpa mtoto wangu mtihani wa kuonesha kiwango chake cha kuelewa Kingereza.
- Singependa idara ya elimu ya mji wa Lynchburg kumpa mtoto wangu mtihani wa kuonesha kiwango chake cha kuelewa Kingereza.

Tafadhali chagua mojawapo kama ungependa mtoto wako apate usaidizi wa masomo ya Kingereza (ESL).

- Ningependa mtoto wangu apate usaidizi wa Kingereza baada ya darasa za kawaida.
- Singependa mtoto wangu apate usaidizi wa Kingereza baada ya darasa za kawaida. Naelewa ya kwamba, kukataa usaidizi wa masomo ya Kingereza (ESL), mwalimu wa mtoto wangu kwa masomo ya kawaida, halazimiki kumpa mtoto wangu usaidizi usio sawa na wanafunzi wenzio wanao elewa Kingereza kama lugha yao ya mama.

Sign

_____/_____
Tarehe